



*Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482*

# KARAMU YA BWANA WETU

Bwana wetu aliwaagiza wanafunzi wake wafanye jambo moja tu ili wamkumbuke:

*"Bwana Yesu, usiku ule aliotolewa, alitwaa mkate, na akiisha kushukuru, akaumega, akasema, Huu ndio mwili wangu ulio kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa kunikumbuka. Vivyo hivyo, baada ya kula akakitwaa kikombe, akisema, Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu; fanyeni hivi, kila mnywapo, kwa kunikumbuka. Maana kila mwalapo mkate huu, na kunywa kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata atakapokuja."*
(*1 Wakorintho 11:23-26*)

Ibada hii, ambayo kwa wanafunzi wa Biblia hujulikana kama **Ukumbusho wa Bwana**, ni kumbukumbu ya tukio lile ambapo Bwana, akiwa katika chumba cha juu pamoja na wanafunzi wake, alianzisha ibada hii takatifu kwa ajili ya Kanisa—mwili wa Kristo. Hebu tuchunguze kwa undani ibada hii na maana yake ya rohoni.

*"Jitakaseni na kuondoa chachu ya kale, mpate kuwa donge jipya, kama vile mlivyo bila chachu. Maana pasaka wetu, yaani Kristo, amekwisha kutolewa kuwa sadaka yetu."*(*1 Wakorintho 5:7*)

Ili tuelewe jinsi Kristo alivyo Pasaka wetu, ni lazima kwanza tusome kuhusu Pasaka ya kwanza:

*"Bwana akamwambia Musa na Haruni katika nchi ya Misri, Mwezi huu utakuwa mwanzo wa miezi kwenu; ni mwezi wa kwanza wa mwaka kwenu. Waambieni kusanyiko lote la Israeli, katika siku ya kumi ya mwezi huu, kila mtu atwae mwana-kondoo kwa jamaa zake, mwana-kondoo mmoja kwa kila nyumba. Na ikiwa watu wa nyumba ni wachache kwa mwana-kondoo mmoja, basi yeye na jirani yake wa karibu waichukue pamoja mwana-kondoo huyo, kulingana na hesabu ya watu; kwa kadiri ya ulaji wa kila mtu, ndivyo mtakavyomhesabu kwa mwana-kondoo. Mwana-kondoo wenu atakuwa wa mwaka mmoja, mume asiye na ila, nanyi mtaweza kumchukua katika kondoo au katika mbuzi. Mtamtunza hata siku ya kumi na nne ya mwezi huu, ndipo kusanyiko lote la jamii ya Israeli watamchinja jioni. Nao watatwaa baadhi ya damu hiyo na kuitia katika miimo ya milango na juu ya miimo ya milango ya nyumba ambazo watamla. Watamla nyama usiku huo ule, wakiichoma kwa moto, pamoja na mboga za majani machungu, na mikate isiyotiwa chachu. Msile nyama hiyo mbichi, wala iliyochemshwa kwa maji, bali iliyochomwa kwa moto; kichwa chake, miguu yake na matumbo yake. Wala msisaze yoyote mpaka asubuhi; na kama ikisalia mpaka asubuhi, mtachoma kwa moto. Nanyi mtamla hivi: viuno vyenu vitakuwa vimefungwa, viatu miguuni mwenu, na fimbo mikononi mwenu; nanyi mtamla kwa haraka; ni Pasaka ya Bwana. Maana usiku huo nitapita katikati ya nchi ya Misri, na kuwapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, wa watu na wa wanyama; nami nitatoa hukumu juu ya miungu yote ya Misri; Mimi ndimi Bwana."* (*Kutoka 12:1-12*)



Kushika Pasaka mara moja kila mwaka lilikuwa agizo, na ndiyo sheria ya kwanza kabisa aliyowapa Mungu Waisraeli kupitia kwa Musa.

Pasaka hii ilifanyika katika mwezi wa kwanza wa mwaka mpya wa Israeli—unaojulikana leo kama **mwezi wa Nisan**. Mwana-kondoo alichaguliwa siku ya kumi na akatunzwa hadi siku ya kumi na nne; kisha akachinjwa wakati wa jioni. Damu yake iliwekwa kwenye miimo ya milango ya nyumba. Nyama iliokwa na kuliwa usiku huo huo, si mbichi wala ya kuchemshwa. Iliambatana na mboga chungu na mikate isiyo na chachu. Kilichosalia asubuhi kiliteketezwa kwa moto. Walioila walitakiwa wawe wamevaa kikamilifu—viatu, fimbo na nguo zao—kwa kuwa walikuwa tayari kwa safari. Waliamriwa wale kwa haraka kwa sababu: ***"ni Pasaka ya Bwana**."*

Tunajua kuwa *"torati ni kivuli tu cha mema yatakayokuja, si sura halisi ya mambo hayo."*(*Waebrania 10:1*). Torati ilijaa mifano ya mambo yanayomhusu Kristo—na hata Pasaka ilikuwa mfano wa hayo.

Mwana-kondoo aliwakilisha **Bwana wetu Yesu Kristo**, ambaye ni kichwa cha kanisa—mwili wake. Mtume Paulo aliandika:

*"Maana Kristo, Pasaka yetu, amekwisha kutolewa sadaka kwa ajili yetu."* (*1 Wakorintho 5:7*)

Mwana-kondoo alikuwa wa kuangaliwa kuanzia siku ya kumi hadi ya kumi na nne—huu ni mfano wa huduma ya Bwana wetu kwa *"nyumba ya Israeli"*. Kipindi hicho kilikuwa nusu ya "wiki ya kinabii" ya miaka saba halisi:

*"Naye atafanya agano imara na watu wengi kwa muda wa juma moja; na katikati ya juma atakomesha dhabihu na sadaka."*(*Danieli 9:27*)

Kuchinjwa kwa mwana-kondoo jioni ya siku ya nne ni mfano wa **kifo cha Bwana wetu** katikati ya mwaka wa nne, saa ya tisa ya mchana:

*"Na yapata saa ya tisa Yesu alipaza sauti kwa nguvu … naye akatoa roho yake."*
(*Mathayo 27:46,50*). Kwa Wayahudi, saa ya tisa ilikuwa saa 9 alasiri.

Wayahudi walitumia damu kuipaka kwenye miimo ya milango ya nyumba zao. Kwa Wakristo, hii ni ishara ya **neema ya Bwana** inayowekwa juu ya *milango ya mioyo yetu*—kwa kuwa mlango unawakilisha moyo:*"Tazama, nasimama mlangoni nabisha …"* (*Ufunuo 3:20*)

Hivyo basi, Waisraeli wa rohoni—*"nyumba ya imani"*—wanapokea kifuniko cha damu ya Yesu juu ya mioyo yao:

*"Mioyo yetu imekwisha kunyunyizwa ili iwe safi na dhamiri mbaya, na miili yetu imeoshwa kwa maji safi."*(*Waebrania 10:22*)

.
Hii ni picha nzuri ya **kuhesabiwa haki na msamaha wa dhambi** kupitia damu ya Yesu, sadaka yake ya fidia msalabani.

Yote haya yalifanyika *"usiku"*—kwa maana:*"Kilio huja kukaa usiku, lakini furaha huja asubuhi."* (*Zaburi 30:5*). Huu ni **usiku wa sasa** kabla ya *"asubuhi" ya Ufalme wa Mungu*.

Kauli *"ikiwa imechomwa kwa moto"* ni ishara ya mateso, majaribu, na dhiki zote alizovumilia Mwokozi wetu wakati alipokuwa *katika mwili*. Amri ya kutokubakiza chochote ifikapo asubuhi inamaanisha kuwa **wanafunzi wake wote wanapaswa kuishi maisha yanayofuata kabisa hatua zake**:

*"Maana mliitwa kwa ajili ya hayo; kwa kuwa Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia mfano, ili mfuate nyayo zake."*(*1 Petro 2:21*)

Nyama ya mwana-kondoo ililiwa pamoja na *"mboga za majani machungu na mikate isiyotiwa chachu"*(*Kutoka 12:8*). **Mikate isiyotiwa chachu** inawakilisha **Neno la Kweli lililo safi**. **Mboga chungu** zinawakilisha **majaribu na dhiki za kila siku** tunazopitia tunapotaka kutembea katika *nuru*, ilhali waliotuzunguka wanaishi katika *giza la ulimwengu huu*: *"Naam, wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa."*(*2 Timotheo 3:12*) *"Huwafuata Mwana-Kondoo kila aendapo."* (*Ufunuo 14:4*)

Nyama haikupaswa kuliwa ikiwa imechemshwa au mbichi. Tunaelewa kwamba **mateso ya Bwana wetu Yesu Kristo**, *"mtu Kristo Yesu"*, yanaonyeshwa vizuri zaidi kwa **kuchomwa kwa moto**.

Katika kila mchakato wa upishi, hutumika **moto**—ambao ni mfano wa **dhiki na mateso**. Lakini moto wa kuchoma ni mkali zaidi kuliko wa kuchemsha.Kuchoma nyama kunahitaji **joto mara mbili ya kuchemsha**, na hivyo huonyesha **kiasi kikubwa cha mateso** aliyoyavumilia Kristo.

Waliamriwa *“msisaze yoyote mpaka asubuhi”*
(*Kutoka 12:10*).
Hii inafundisha kuwa wito huu wa juu wa **kushiriki mateso ya Kristo** na **kufa pamoja naye** ni wa kipindi cha *usiku* wa Enzi hii ya Injili.
Fursa hii ya thamani sana **haitapatikana tena asubuhi ya Enzi ya Milenia**, wakati mwili wa Kristo utakapokuwa **umekamilika na kutukuzwa**.

Hapo ndipo *“jua la haki litakapochomoza lenye tiba katika mbawa zake”* (*Malaki 4:2*).

Fursa hii ya kipekee ya kushiriki katika mateso ya Kristo **haitarudiwa tena milele**. Kama mtume Paulo alivyosema: *“Tutapataje kupona sisi tusipoujali wokovu mkuu namna hii?”* (*Waebrania 2:3*)

Wokovu huu wa mbinguni, wa kufikia **asili ya kimungu ya utukufu**, utatamatika mwisho wa Enzi ya Injili. “Asubuhi” ya Enzi ya Milenia itaashiria **kuanza kwa wokovu wa wanadamu waliobaki**, yaani **wokovu wa kidunia**.

Ndiyo maana nyama iliyochomwa—mfano wa wokovu wa Kikristo—ilitakiwa **iteketezwe kabisa**, kuonyesha kwamba *“mlango wa wokovu huu wa utukufu umefungwa milele.”*

*“Mtalila hivi: Viuno vyenu viwe vimefungwa, viatu miguuni mwenu, na fimbo mikononi mwenu.”*(*Kutoka 12:11*)
Hali hii ya kuvaa kikamilifu—ikiwa na viatu na fimbo—inaonyesha **utayari wa kusafiri**.

Wote walio ndani ya mwili wa Kristo ni **wasafiri wa rohoni**, wakipita *jangwani mwa dunia hii*, wakielekea *Kanaani ya mbinguni*. Yesu alisema:*"Naenda kuwaandalia mahali."*(*Yohana 14:3*)

Wokovu wa Kanisa ni wa **mbinguni**, si wa duniani. Maisha ya sasa ya wafuasi wa Kristo ni **safari ya kuelekea mbinguni**.

Mavazi na viatu vinaashiria *"silaha kamili za Mungu"*:
*"Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ile ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama."*
(*Waefeso 6:13*)
Maelezo ya silaha hizi yanapatikana kuanzia aya ya 14 hadi 17.

Kila mfuasi wa Kristo anapaswa **kuwa na silaha hizi zote**, ikiwa ni pamoja na viatu, ili **kupigana vita vizuri vya imani**.

*Fimbo mkononi* hutukumbusha *fimbo ya mchungaji*: *"Wewe upo pamoja nami; fimbo yako na gongo lako vyanifariji."* (*Zaburi 23:4*)

**Gongo na fimbo** ni faraja kwa Israeli wa rohoni. Hii ni ishara ya *Mfariji* ambaye Yesu alimuahidi:*"Lakini yeye, huyo Roho wa kweli, atakapokuja, atawaongoza awatie kwenye kweli yote … naye atawaonyesha mambo yajayo."*(*Yohana 16:13*)

**Roho wa kweli** ni **Roho Mtakatifu**. Kwa hiyo:

- **Gongo** linawakilisha **Neno la Mungu**
- **Fimbo** inawakilisha **Roho Mtakatifu**

Waliambiwa:*"Mtalila kwa haraka, maana ni Pasaka ya Bwana."* (*Kutoka 12:11*) Hili ndilo hitimisho la maagizo ya ibada hii, likiwa na **fundisho la tabia na mtazamo wa kiroho**.

Inawakilisha **nia na bidii ya Israeli wa rohoni**, wanaposhiriki katika *"wokovu huu mkuu."*Mtume Paulo aliandika: *"Utendeeni wokovu wenu kwa kuogopa na kutetemeka."* (*Wafilipi 2:12*) Hakumaanisha kutetemeka kwa mwili, bali kuwa **uangalifu, wenye bidii na kujichunguza**.

Aliongeza:*"Basi, kwa kuwa ahadi ya kuingia rahani mwake imebakia, na tuogope, asije mmoja wenu akakosa kuifikia." Waebrania 4:1*)

Kila muda ni wa thamani sana kwa walioitikia **wito wa mbinguni** na kuishi maisha ya **kutoa nafsi kwa Kristo**.

Hii ndiyo maana ya kauli: *"Mtlila kwa haraka."*

Wakristo wa leo hawasherehekei Pasaka; wanakumbuka jambo kubwa zaidi: *"Basi na tushike sikukuu."*(*1 Wakorintho 5:8*)

*"Ilipofika saa, Yesu na mitume wake waliketi chakulani. Akawaambia, Nimetamani sana kuila Pasaka hii pamoja nanyi kabla ya kuteswa kwangu. Maana nawaambia, sita ila tena hata itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu. Akakitwaa kikombe, akashukuru, akasema, Itwaeni hiki, mkigawanye ninyi kwa ninyi. Maana nawaambia, sitakunywa tena tangu sasa uzao wa mzabibu, hata ufalme wa Mungu utakapokuja. Akatwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa, akisema, Huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa kunikumbuka."* (*Luka 22:14-19*)

Yesu akawa Mwana-Kondoo wa Mungu wa mfano mkuu, aliyetimiza mfano wa kifo cha mwana-kondoo wa Pasaka. Katika karamu hiyo ya mwisho aliweka alama mpya za "**mkate" na "divai."**

*"Akakitwaa kikombe, akashukuru, akasema, Itwaeni hiki, mkigawanye ninyi kwa ninyi; naye akatwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa, akisema, Huu ndio mwili wangu, unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa kunikumbuka."*(*Luka 22:17,19*)

Bwana aliwaalika wanafunzi wake kula mkate na kunywa divai. Hii ni mwaliko kwa kundi la kanisa kushiriki katika mateso yake, kumfuata hata hadi mauti.

Heshima hii ya kushiriki katika mateso ya Bwana imetajwa na mtume Paulo:
*"Nafurahi kwa mambo niliyoteseka kwa ajili yenu, nami natimiliza katika mwili wangu yaliyopungua katika mateso ya Kristo kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa."*(*Wakolosai 1:24*)

Paulo alieleza heshima ya kushiriki katika *mateso ya Kristo*. Alieleza pia kuwa ni kama mtu kuzamishwa katika mauti ya Kristo: *"Hamjui ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake?"*(*Warumi 6:3*)

Ingawa Yesu *alibatizwa katika mauti*, haikuwa kwa sababu ya dhambi yake mwenyewe. Kifo chake kilikuwa ni cha dhabihu kwa ajili ya dhambi za ulimwengu:*"Na baada ya majuma sitini na mawili, Masihi atakatiliwa mbali, wala hatakuwa na kitu."*(*Danieli 9:26*)

Vivyo hivyo, Wakristo sasa wameitwa kutoa maisha yao ya kibinadamu katika mauti ya dhabihu kwa ajili ya wengine: *"Basi, ndugu zangu, nawasihi kwa rehema zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu ya kiroho."*(*Warumi 12:1*)

Dhabihu hii ni *takatifu* kwa sababu ya kuhesabiwa haki kunakotolewa kwa *vazi la haki*:*"Ameniuvika vazi la wokovu, amenifunika kwa joho la haki."*(*Isaya 61:10*)

Dhabihu hii hudumishwa kwa maungamo ya mara kwa mara wa dhambi:
*"Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atusamehe dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote."*(*1 Yohana 1:9*)

Hii ndiyo heshima kubwa ya kufuata nyayo za Bwana hadi kwenye mauti ya dhabihu. Hii pia ndiyo meza ya ushirika wa mwili wa Kristo, jambo ambalo ni fumbo kwa dunia:

*"Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twashiriki mkate mmoja."*(*1 Wakorintho 10:17*)

Hii ni picha ya umoja wa mwili wa Kristo, ambao, ingawa una washiriki wengi, bado ni mmoja:*"Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu."*(*Waefeso 4:4*)*"Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja."*(*Waefeso 4:5*)

Ubatizo huu mmoja si wa kuzamishwa majini tu, ambao ni ishara tu. Una maana ya kina zaidi. Bwana aliwauliza wanafunzi wake wawili, *"Mwaweza kunywea kikombe ninachokinywea, au kubatizwa kwa ubatizo ninaobatizwa?"*Wakamwambia, Tunaweza. Yesu akawaambia, *"Hakika mtakinywea kikombe nilichokinywea, na kubatizwa kwa ubatizo ninaobatizwa."*(*Marko 10:38-39*)

Wanafunzi wote wa Bwana wamepewa heshima ya kuingia katika umoja wa ubatizo huu mmoja ndani ya mauti ya Bwana. Kwa hiyo, kila mara Ukumbusho unapoadhimishwa, alama zinazotumika ni *"mkate mmoja"* na *"kikombe kimoja."*

Paulo aliandika:*"Lakini mtu na ajitathimini nafsi yake, na hivyo aule mkate, na kuinywea kikombe. Kwa maana yeye alaye na kuinywea bila kutambua mwili wa Bwana, hujiletea hukumu juu yake mwenyewe."* (*1 Wakorintho 11:28-29*)

Hii inaeleza juu ya kujichunguza—mtazamo wa moyo na hali ya ndani—kila wakati mtu anaposhiriki katika alama hizi takatifu, akikumbuka agano lake mwenyewe la kushiriki katika mateso na kifo cha dhabihu cha Kristo, na namna ambavyo amekuwa mwaminifu katika kulitimiza. Ni washiriki waliotoa maisha yao na walioko katika

agano tu ndio wanaopaswa kushiriki.Kila mmoja ni kwa ajili yake mwenyewe kupima jambo hili:*"Lakini mtu na ajitathimini nafsi yake."* *"Kwa maana kila mwalapo mkate huu, na kunywa kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata atakapokuja."*(*1 Wakorintho 11:26*)

Wengine hudhani kuwa maneno *"kila mwalapo"* yana maana ya kufanya hivyo wakati wowote, hata mara nyingi kwa siku kama wafanyavyo Wakatoliki wa Kirumi.Kwa makanisa ya Kiprostanti, kuadhimisha kila mwezi au kila wiki ni jambo la kawaida. Ingawa ibada hii takatifu ilipaswa kuwa *"karamu ya jioni,"* ifanyike usiku baada ya jua kuzama, makanisa ya Kikristo huifanya wakati wowote wa mchana au usiku.

Hata hivyo, kauli *"kila mwalapo"* inapaswa kueleweka katika muktadha wa **Pasaka ya Kiyahudi**, ambayo Wayahudi waliadhimisha kila mwaka katika tarehe maalum ya kalenda yao.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake,*"Fanyeni hivi kwa kunikumbuka."* Ukumbusho huu ni kumbukumbu ya kifo cha Bwana, na ni jambo la mantiki kwamba uadhimishwe **mara moja kwa mwaka**, katika **tarehe ile ile ya kalenda** ambayo Bwana aliweka ibada hii, ambayo ilikuwa siku ya kumi na nne ya mwezi wa Nisan:

*"Mtawatunza hata siku ya kumi na nne ya mwezi huu, ndipo jamii yote ya Israeli itamchinja jioni."*(*Kutoka 12:6*)

Zaidi ya hayo, tunasoma kuwa mwana-kondoo wa Pasaka wa mfano alichinjwa jioni. Mfano huo ulitimizwa na **kifo cha Yesu msalabani** kama Mwana-Kondoo wa Mungu saa 9 alasiri (*saa ya tisa*). Lakini aliweka Ukumbusho huo takribani saa 20 kabla ya hapo, **baada ya saa 12 jioni (6:00 PM)** katika Nisan 14.

Tarehe hiyo tunaiweka kwa kuangalia **kalenda ya Kiyahudi**, tukijua kuwa baada ya jua kuzama, Wayahudi huanza siku mpya ya hesabu.

Hapo ndipo Bwana aliweka Ukumbusho wa kwanza na kuwaagiza wafuasi wake **waumkumbuke kwa wakati huo kila mwaka.**

Hapa chini ni **tarehe za Ukumbusho** kwa miaka 18 ijayo:

Kwa wote wanaoshiriki Ukumbusho huu kuna onyo kali:*"Hamwezi kunywea kikombe cha Bwana na kikombe cha mashetani; hamwezi kuwa na sehemu katika meza ya Bwana na meza yamashetani."*(*1 Wakorintho 10:21*)

Hii inahusu kuchanganya Roho Mtakatifu anayemfanya mtu kuwa wa Mungu, na roho ya dunia: *"Kutoka kinywa kimoja hutoka baraka na laana. Ndugu zangu, haipaswi kuwa hivi. Je, chemchemi moja yawweza kutoa maji matamu na maji machungu kwa wakati mmoja?"* (*Yakobo 3:10-11*)

Wale waliopokea Roho Mtakatifu lazima wafanye kila jitihada **kupinga na kushinda matendo ya roho ya kidunia**. Mtume Paulo aliorodhesha baadhi ya hayo:*"Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya; uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, uzushi, faraka, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo; nawambia mapema, kama nilivyokwisha kusema tangu zamani, ya kwamba wale watendao mambo hayo hawataurithi ufalme wa Mungu."*(*Wagalatia 5:19-21*)

**TAREHE ZA UKUMBUSHO KWA MIAKA 20**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2012 | Aprili | 5 | Alhamisi |
| 2013 | Machi | 24 | Jumapili |
| 2014 | Aprili | 13 | Jumapili |
| 2015 | Aprili | 2 | Alhamisi |
| 2016 | Aprili | 21 | Alhamisi |
| 2017 | Aprili | 9 | Jumapili |
| 2018 | Machi | 29 | Alhamisi |
| 2019 | Aprili | 18 | Alhamisi |
| 2020 | Aprili | 7 | Jumanne |
| 2021 | Machi | 26 | Ijumaa |
| 2022 | Aprili | 14 | Alhamisi |
| 2023 | Aprili | 4 | Jumanne |
| 2024 | Aprili | 21 | Jumapili |
| 2025 | Aprili | 11 | Ijumaa |
| 2026 | Machi | 31 | Jumanne |
| 2027 | Aprili | 20 | Jumanne |
| 2028 | Aprili | 9 | Jumapili |
| 2030 | Machi | 29 | Alhamisi |

Wanaoshiriki Ukumbusho hawapaswi kulisahau jambo hili.

Kanisa la kwanza lilikuwa na kawaida ya kukutana mara kwa mara *"kumega mkate."* Kwa mfano: *"Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana kuvunja mkate, Paulo aliwahutubia wale waliokuwa wamekusanyika, kwa kuwa alikusudia kusafiri kesho yake; akaendelea kusema hadi usiku wa manane."*(*Matendo 20:7*)

Hii haikuwa sherehe ya Ukumbusho wa Bwana. Baada ya kufufuka kwake, Yesu aliwamegea mkate wanafunzi wake: *"Ikawa alipokuwa ameketi nao chakulani, alitwaa mkate, akabariki, akaumega, akawapa."*(*Luka 24:30*)

Hii hakika haikuwa Pasaka. Ilikuwa ni mlo wa kawaida wa jioni. Ilikuwa desturi ya Kiyahudi kutoa shukrani kwa Mungu kabla ya kula. Kisha mkate ulimegwa vipande ili uwe rahisi kuliwa. Hivyo ndivyo Yesu alivyofanya: *"Alichukua mkate, akashukuru, akaumega, akaanza kuwapa."*

Kwa hiyo, kauli hiyo inapaswa kueleweka kuwa ndugu walikula pamoja. Lilikuwa ni wakati wa **ushirika na upendo**, na halikuhusiana kabisa na adhimisho la Ukumbusho wa Bwana.

Wengine wamekuwa na maswali kuhusu kauli: *"Mwaitangaza mauti ya Bwana hata atakapokuja."*(*1 Wakorintho 11:26*)

Kwa kuwa tunaamini kuwa Bwana alikuja kwa namna isiyoonekana mwaka 1874, je, tunapaswa kuendelea kuadhimisha Ukumbusho?

Yesu alisema:*"Nawaambia, sita ila tena mpaka itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu."*(*Luka 22:16*)

Utimilifu wa kushiriki mkate ni ndani ya **ufalme wa Mungu**. Sehemu ya mwili wa Kristo bado ipo *katika mwili* hata baada ya kurudi kwa Bwana na kuanza kwa awamu isiyoonekana ya ufalme mwaka 1874 (*1 Wathesalonike 4:17*). Hadi washiriki wote wa mwili wa Kristo

watakapokuwa **wametukuzwa**, kila mmoja ataendelea kushiriki mkate na kuadhimisha Ukumbusho wa Bwana.

Kauli *"mwitangaza mauti ya Bwana hata atakapokuja"* ina maana dhahiri ya *"kuja kwake katika utukufu wa ufalme wa Mungu"*.


Hii ni wakati*"Mwana wa Adamu atakapokuja katika utukufu wake, na malaika wote pamoja naye …"*(*Mathayo 25:31*)

Huu ndio wakati ambapo **kanisa lote litakuwa limekamilika na kutukuzwa**.

Ukumbusho wa kifo cha Bwana wetu utaendelea kuadhimishwa na wale waaminifu wanaomfuata kwa nyayo zake **maadamu bado wako katika mwili.**

Mpaka wakati huo, **na tushike sikukuu**:
*"basi na tuifanye karamu…"*
(*1 Wakorintho 5:8*)

═✿═✿═✿═*Amina*═✿═✿═✿═



*Kwa Masomo zaidi Tuandikie Ujumbe kupitia:*

*Email: thekingdom1_6@gmail.com au isayaruhala25@gmail.com*

*©HAKIUZWI*

***Namba ya Whatsap: 0752965019/ +255 757 411 482***